# Jarida la UQAB

Toleo 1
Februari 2017 Miladi
Jumada Al Awwal 1438 AH

Elimu Chini Ya Mfumo Wa Urasilimali Haiwezi Kufanyiwa Marekebisho

Pengo Kati ya Matajiri na Masikini Linazidi

Chaguzi za Kidemokrasia Hudunisha Hadhi ya Wanawake

Siku ya Ukoma duniani: Hadaa nyengine ya Kibepari



# Viongozi Wanang'ang'ania Uongozi Huku Raia Wakifa Njaa!



# Viongozi Wanang'ang'ania Uongozi Huku Raia Wakifa Njaa!

**Taarifa Kwa Vyombo Vya Habari**

Harakati ya Kiislamu ya Hizb ut-Tahrir Kenya inasikitishwa mno na mamilioni ya raia wanaokumbwa na baa la njaa. Inahuzunisha kuona picha za wazee madhaifu wanaoshindwa kusimama huku watoto wakililia mama zao kwa sababu ya njaa! Kwa masikitiko makubwa huku hali hii ya kutamausha ikionekana, wanasiasa wa pande zote (serikalini na upinzani) wanazunguka huku na kule wakitoa maneno matupu na kuwinda kura za uchaguzi wa Agosti mwaka huu!

Tunaeleza bayana kuwa njaa hii haijasababishwa tu na ukame kama inavyodaiwa na wadau wa serikali bali hasa ni utepetevu wa kiserikali na kutelekeza/kudharau jukumu la kusimamia raia wake. Dalili ya haya ni kuwa watabiri wa hali ya hewa walitoa onyo mapema juu ya hali hii lakini serikali ikajitia hamnazo.


Kenya ina rasimali za kutosha ikiwemo madini, mito na ardhi kubwa yenye rutuba lakini kwa sababu ya sera mbovu za mfumo wa kiuchumi wa kibepari, utajiri huu wote humilikiwa na mabwenyenye wachache wanaojinufaisha huku raia wa kawaida wakiambulia patupu! Kihakika serikali inayowajibika kikweli na kuwa na nia ya kuondosha njaa kikweli hutakikana kuekeza zaidi katika sekta ya kilimo na wala sio kutegemea uagizaji wa vyakula kutoka mataifa ya nje ama kutegemea misaada ya kigeni. Serikali ya kikweli iliyo na nia kweli ya kuondosha umasikini ungeikuta ikiimarisha kilimo kwa kuja na mikakati kama kuwanunulia wakulima mbolea na kuwapa pesa za kutayarisha mashamba yao, kuweka miradi ya unyunyizaji wa mashamba. Mikakati hii ndio hudhaminia raia usalama wa chakula. Kwa bahati mbaya, haya hayafanyiki kwenye tawala zinazojifunga na mfumo wa kirasilimali ambapo wanasiasa wake hupuuza kusudi mikakati hiyo badali yake hunufaika kila kunapotokea baa la njaa kwa kudhibiti biashara za uagizaji wa mahindi na bei ya unga wa mahindi hupanda zaidi.

Tunatamatisha kwa kuwaomba matajiri wote wa Kiislamu na wasokuwa wa Kiislamu kufanya juhudi maradufu kusaidia waathiriwa wa baa la njaa. Twapenda wakati huo huo kuikumbusha jamii ya Kenya kusimama wazi kufichua maovu ya urasilimali na wanasiasa wake wanaong'ang'ania tu uongozi wapate kushibisha matumbo yao.Sisi tunaamini kuwa mfumo wa Uislamu ukitabikishwa/ukitekelezwa chini ya utawala wa Khilafah utamwezesha kiongozi kugawanya na kuzipeleka rasilimali hadi katika maeneo kame. Hivi ndivyo hali ilivyokuwa katika utawala wa Umar bin Khattab (ra) ambaye chini ya utawala wake aliwajibika kama kiongozi na kukabiliana ukame. Umar (ra), aliandikia barua magavana wake wa maeneo ya Misri, Sham, Palestina na Iraq akiwataka kuleta msaada wa chakula nao wakafanya hivyo pasina kusita hadi mamia ya raia wakaokolewa kutokana na baa la njaa.

**Shabani Mwalimu**

**Mwakilishi kwa Vyombo vya Habari Hizb ut-Tahrir Kenya**






# Elimu Chini Ya Mfumo Wa Urasilimali Haiwezi Kufanyiwa Marekebisho

Kumekuwa na vilio vya kudai 'mabadiliko katika sekta ya elimu' ndani ya Kenya tangu Fred Matiang'i alipochukua hatamu katika Wizara ya Elimu mwaka jana. Amejitahidi kwa kiasi fulani kujaribu kuondosha muozo uliokuwa unaikumba nidhamu ya mitihani nchini. Ama kuwa amefaulu au la hilo ni suala la kujadiliwa siku nyingine. La muhimu ni ndani ya muhula huu kunatarajiwa kuanza rasmi kwa mtaala mpya wa elimu; ambao unatarajiwa kuchukua nafasi ya ule unao kashifiwa wa 8-4-4. Mpangilio huu ambao umetumika kwa miongo mitatu uliweka miaka minane kwa elimu ya msingi, miaka mine kwa elimu ya shule ya upili na kwa miaka mine kwa elimu ya chuo kikuu. Kwa sababu hiyo mtaala huo ukachukua mahala pa mtaala wa 7-4-2-3 ambao ulikuwa unashtumiwa kuwa ni wa kikoloni na unaochangia kuwepo kwa matabaka. Ripoti kutoka kwa Taasisi ya Mitaala ya Elimu Kenya (KICD) inaashiria kuwa mtaala mpya umepangilia ngazi tatu; Elimu ya Miaka ya Mwanzo, Elimu ya Katikati na Elimu ya Wakuu. Hata hivyo imependekeza kuwepo mpangilio wa 2-6-3-3-3 wa elimu ambao wanasema utahakikisha wasomi wanapata uwezo na taaluma ya kuweza kufikia matarajio ya uajiri ndani ya Ruwaza 2030. Mkurugenzi wa KICD Juliua Jwan alisema kuwa "mtaala huo utapunguza mzigo na utabadilisha mpangilio wa kusoma na kuwafanya wasomi waweze kujitambua kwa misingi ya Demokrasia ya taifa hili, kitu ambacho mtaala uliopo sasa haujatatua" (Daily Nation ya 1 January, 2017)

Lawama na vilio vilishamiri punde tu baada ya kutangazwa matokeo ya Mtihani wa Shule za Upili ya Kitaifa (KCSE) ya Mwaka 2016. Hii inaashiria hali mbili yawezekana kuwa ni ukweli kutoka kwa washika dau wanaoijali sekta ya elimu au ikawa ni magenge ya wezi wa mitihani wakijaribu kulipiza kisasi. Kama ilivyoripotiwa na gazeti la Daily Nation la 3 Januari, 2017, kuwa Muungano wa Walimu wa Baada ya Shule za Msingi (KUPPET) kupitia Katibu Mkuu – Akello Misori ameyakosoa matokeo ya KCSE yaliyotolewa Disemba. Alisema kuwa; "hali ya kawaida ilitarajiwa kuonyesha waliopita wachache na idadi kama hiyo ikiwa chini, na wengi wakiwa katikati. Hali isiyokuwa ya kawaida imeashiria kuwa matokeo ya 2016 sio ya kutegemewa." Akaongezea kusema kuwa walimu watataka uchunguzi ufanywe juu ya kutayarishwa mitihani na hali ya ilivyo ilivyomakiwa/alama zilivyopeanwa. Hii ni baada ya malalamishi kutolewa kuwa mitihani ilimakiwa haraka haraka.

Muhanga mwingine katika matoleo hayo ni mpango wa shahada za sambamba (Parallel Degree Programmes) ambao unapatikana katika vyuo vikuu. Fred Matiang'I alitangaza kuwa vyuo vikuu vya umma vitachukua moja kwa moja wanafunzi wote 88,929 waliopata alama ya C+ na zaidi katika KCSE. Zaidi ya wanafunzi 44,000 waliopata C na walitarajia kujiunga na vyuo vikuu kupitia mpango wa shahada za sambamba au kujiunga katika taasisi za kibinafsi wametupwa nje ya mipango ya shahada baada ya ishara za mapema kuwa alama za kuchaguliwa kusomea kozi tofauti tofauti hazitapunguzwa. Kozi hizi zimetumika na vyuo vikuu kupata mabilioni ya fedha kutokana na wanafunzi wengi kutopata nafasi za kujiunga na vyuo vikuu vya umma kupitia mpango wa kawaida wa usajili. Vyuo vikuu vimetumia rasilimali nyingi idadi kubwa ikiwa zimekopwa ili kubuni matawi ya vyuo hivyo ili kuweza kutosheleza mahitaji ya elimu ya juu yanayoongezeka kila mwaka kutoka na kujisajili maelfu ya watu kwa masomo ya jioni.Kwa mfano katika mtihani wa KCSE wa 2015 wanafunzi 165,766 walipata alama ya CT na zaidi zilizo watosheleza kujiunga chuo kikuu. Hata hivyo ni wanafunzi 74,384 pekee waliochaguliwa kujiunga na vyuo vikuu vya umma kutokana na uhaba wa nafasi hivyo kupelekea wanafunzi 91,377 kujiunga katika vyuo vya kibinafsi. Ikiwa idadi kubwa ya taasisi za elimu ya juu, hususan zile zinazojulikana kama matawi yaliyobuniwa na vyuo vya umma na kibinafsi; ni wazi kuwa yako ili kutapeli maanake yako hapo kwa msingi wa kufanya biashara tu na si kama taasisi za kusomesha.

Ni wazi kuwa kwa muda mrefu sasa

*endelea ukurasa 4*

kutoka ukurasa 3

tumekuwa na nidhamu ya kiujanja ya mitihani ambapo uizi wa mitihani umekuwa ni jambo la kawaida. Shule, wazazi na walimu wamekuwa wakishirikiana na maofisaa wa Baraza la Mitihani la Kitaifa (KNEC) kuiba mitihani. Ambayo hatima yake ni kupatikana kwa alama nyingi za juu ambazo haziwezi kuhimili vipimo. Ushahidi ulikuwa umeanza kuwa mwingi ukiashiria kuwa watahiniwa wengi waliopata alama nyingi wanaanguka wanapofika chuo kikuu. Nusu ya wanafunzi zaidi ya 50,000 ya wanaohitimu shahada kila mwaka ndio wanaotimiza viwango vya ajira. Na nusu ya wanaotimiza viwango hivyo haviambatani vigezo hivyo haviambatani na taaluma walizosomea. Baraza la Baina ya Vyuo Vikuu la Afrika Mashariki (IUCEA) ilibainisha kuwa katika utafiti uliofanyika 2014. Matokeo ya utafiti huo yalionyesha kuwa idadi kubwa ya wanaohitimu hawawezi kupata au watapata changamoto katika kupata ajira ya kudumu katika sekta walizosomea. Prof Kubasu, amabye ni mwanaelimu alisema kuwa “Hiyo ni sehemu moja ya shida. Nidhamu nzima ya elimu inatakiwa kufikiriwa tena. Hatuna tena motisha ya kutafuta elimu isipokuwa ni uchu wa kutafuta makaratasi ili tupate ajira. Kwa walimu, ni jambo lakutengeneza fedha nyingi kutoka kwa vyuo vikuu wawezavyo.”https://www.standardmedia.co.ke/article/2000123982/only-half-of-university-graduates-in-kenya-are-ready-for-job-market-study-says.


Suali msingi kwetu kujiuliza ni malengo ya elimu yanatimizwa? Twaona mabadiliko au ni mbinu tu zinatumika kuutuliza umma unahangaika kwa kuuliza masuali? Fikra ya kina inaonyesha kuwa hakuna malengo maalumu yanayofikiwa zaidi ya kutoa waliohitimu kwa viwango vya chini. Mabadiliko pia hayawezikani kutokea katika nidhamu fisadi mpaka mpaka nidhamu yenyewe ifanyiwe mabadiliko. Mabadiliko ya Elimu katika mfumo wa Urasilimali ni vigumu kufanyika kwa hiyo ni vigumu kuyanasibisha na matokeo. Waweza kuwekeza katika elimu bora kwa madaktari lakini haimaanishi kuwa utapata nidhamu nzuri ya huduma ya afya.


Kwa mujibu wa Serikali ya Kiislamu inayotarajiwa kusimamishwa kwa njia ya Utume; sera yake ya elimu kipengele 166 ndani ya kielelezo cha katiba yake kinasema, “ Lengo la elimu ni kujenga muonekano wa kiislamu kifikra na kitabia. Hivyo masomo yote ndani ya mtaala yatakuwa juu ya msingi huu”

Na katika nidhamu ya elimu imeandikwa “Elimu ndio njia ya kuhifadhi tamaduni ya umma ndani ya mioyo ya watoto wake na katika kurasa za vitabu vyake, ima ni katika yaliyomo au yasiyokuwemo ndani ya mtaala. Mtaala wa elimu unamaanisha elimu itapangiliwa kwa mujibu wa sera na kanuni za serikali; na serikali ikiwajibika katika kuitekeleza mfano kuweka umri wa kuanza, masomo na njia ya kusomesha. Ilhali elimu isiyokuwa lazima inawachiwa Waislamu kufunza katika majumba, misikiti, vilabu, kupitia vyombo vya habari na majarida n.k bila kulazimishwa kufuata mpangilio au kanuni zinazofungamana na mtaala wa elimu. Kwa hali zote mbili, hata hivyo Serikali ina jukumu la kuhakikisha kuwa fikra na maarifa yanayofundishwa ima yanatokana na Fikra Msingi ya Uislamu au yamejengwa juu yake.”

Haya ndiyo mabadiliko ya kina yanayoweza kuchukuliwa ili kubadilisha nidhamu ya elimu kutoka katika mfumo wa Urasilimali ambao hauna madhumuni wala maadili bali una tegemea zaidi hisia za kizalendo za serikali. Ni hadi pale umma utakapokubali kuwa mabadiliko makubwa wanayoweza kuyafurahia matunda yake ni kupitia elimu ya kweli ambao mwanzo kabisa ni iwafunze kumtambua Muumba wao. Kisha imfunze mwanadamu lengo la kuumbwa kwake, wapi ametoka, yuko wapi na mwisho kabisa yuwaenda wapi. Haya ndiyo mabadiliko tunayotakiwa tuyatamani.

**Kassim Aggesa**
**Mwanachama Katika Kamati ya Mawasiliano Hizb ut-Tahrir Kenya**






E-mail: uqab@hizb.or.ke

# Pengo Kati ya Matajiri na Masikini Linazidi




Katika jamii yoyote ile ya wanadamu ni maumbile watu kutofautiana katika ustawi wa maisha na daima hukuepukiki kuweko na matajiri na masikini katika jamii. Hata hivyo, katika jamii ya kibepari leo mwanya wa matajiri na masikini hukuzwa na kuwa mkubwa mno hii ni kwa sababu asili ya mfumo huu ni kujali maslahi ya kipote kidogo cha watu. Gazeti la The Standard tarehe 17 Januari, 2017 lilichapisha habari kwenye ukurasa wake wa mbele kuhusu ripoti ya kutamausha ya shirika la Oxfam kuwa watu wa nane (8) duniani ndio wanao miliki utajiri wa watu bilioni 3.6! Hii ina maanisha wanane hawa wanamiliki mali za nusu ya idadi ya watu kote duniani!

Licha ya ukuaji wa kitekenolijia na uundaji wa sera za 'kiustarabu' bado kila kukicha pengo la masikini na matajri linazidi kukuwa zaidi. Baada ya vita vya pili vya Dunia kumalizika mwaka 1945, Marekani iliibuka kuwa na dhahabu nyingi jambo lililoipelekea kuhifadhi thamani ya sarafu yake ya dollar kwa dhahabu jambo lililofanya nchi nyingi nazo kuhifadhi thamani ya sarafu zao kwa thamani ya sarafu ya dola ya Marekani. Hatua hii iliipa nguvu Marekani kuliko nchi nyengine. Mwaka 1968 baada ya Marekani kujihusisha na vita baridi ilitumia dhahabu nyingi katika vita hivyo kiasi kulazimika kuchapisha pesa za 'fiati' au pesa zisizo kuwa na thamani ya dhahabu na kupelekea dola bilioni 900 hadi dola trilioni 3.5 kuwa katika mzunguko kwa miaka 2. Hali hii iliipelekea Benki Kuu za Serikali ambazo zinatumia sarafu ya dollar ya Marekani kwa thamani ya sarafu zao; kuchapisha pesa za 'Fiat' kuweza kununua dollar. Jambo hili lilipelekea serikali kuchukua hatamu ya usimamizi wa uchumi na sera mpya na nadharia zikaibuka.

Kenya ikiwa moja ya nchi ambazo huhifadhi sarafu yake kutumia dollar ya Marekani haikuachwa katika sera na nadharia za kiuchumi ambazo zilibuniwa na wachache wenye nguvu ili kuhifadhi utajiri wa ambao unaathri kiuchumi.

Hizi ni baadhi ya nadharia zinazotumika katika kuendeleza unyanyasaji wa kiuchumi:-

**Uhaba wa Rasilimali:** Huu ndio msingi wa uchumi ulimwenguni leo unaoashiria kuwa mahitaji ya wanadamu ni mengi na ni yenye kujirudiarudia na ati kuna uhaba wa rasilimali. Kwa hali hudaiwa kuwa rasilimali leo haziwezi kushibisha mahitaji ya watu. Na ili kutatua tatizo hili wanaloliita 'tatizo msingi la kiuchumi' husemwa kuwa juhudi nyingi zaidi ziielekezwe kwa uzalishaji rasilimali. Lakini wapi! Uzalishaji sio tatizo msingi la kiuchumi bali ni usambazaji wa zile rasilimali zinazozalishwa. Kwa mfano hapa Kenya rasilimali nyingi lakini wanaozalisha ni wachache na kubwa zaidi hazisambazwi kwa watu umasikini huzidi kila siku. Rasilimali kama vile ilmenite inayochimbwa huko Pwani Kusini na makampuni ya kibinafsi ya Titanium Base iliweza kupata tani milioni 3 za madini hayo katika kipindi cha Mwezi wa Septemba na Disemba na inayouzwa tani moja kwa bei ya Sh 14000. Hii ikimaanisha kuwa kampuni hiyo iliweza kupata bilioni Ksh 42 ndani ya kipindi cha miezi mitatu 3 lau ingelikuwa ni serikali ingeli jipatia bilioni Ksh.168 ndani ya mwaka mmoja. Kwa mujibu wa habari zilizo peperushwa na shirika la Africa Oil, tathmini huru iliyofanywa na Gaffney, Cline & Associates mwaka 2014 ilikadiria zaidi ya pipa milioni 600 ya madini ya propabeli (2C) ambayo ina thamani ya mabilioni ya dola za Marekani. Mafuta zaidi yamekuwa yakipatikana tokea wakati huo. Zungumzia madini ya magadi kutoka ziwa Magadi kama Fluorspar huko Kerio Valley, Nobium, Lead na Shaba huko Kwale. Si tu madini hayo bali hata ukulima na mengi zaidi ambayo yana uwezo wa kuzalisha mapato mengi yatakayotumika kwa miaka mingi bila kuomba misaada ya nje.

Kwa hiyo nadharia hii iliwekwa ili rasilimali zote ziweze kumilikiwa na mashirika machache yanayomilikiwa na watu binafsi wachache na kuwaacha wengine wakiwa masikini wa kupindukia.

**Kusambaza uchumi:** Nadharia hii inaashiria kuwa wanapopunguziwa ushuru matajiri basi hupelekea kuwaajiri watu wengi zaidi na hivyo kupelekea kukua kwa uchumi wa eneo. Nadharia hii imeyarahisishia makampuni kupata faida zaidi kwa kulipa ushuru kidogo au kutolipa kamwe ilhali mwananchi wa kawaida ana beba mzigo wote wa ushuru ambao una mrud-

*endelea ukurasa 6*

*kutoka ukurasa 5*

isha hatua ya kwanza kila anapojaribu kujikwamua kimaendeleo.

Nadharia hizi na nyenginezo zinategemea mashirika na wadhamini wake ambao huzitumia kuendesha uchumi. Uhaba wa ajira umekuwa kwa asilimia 60 miongoni mwa vijana na wale asilimia 40 walioajiriwa manuafaa yao yanazidi kudidimia. Idadi ya wafanyikazi walio na mpango walio na mpango wa pensheni kwa mujibu wa ajira zinadorora. Zaidi ya wafanyikazi 10,000 mwaka 2016 walisitishwa kazi ndani ya kampuni zaidi ya 20 ikiwa baadhi yao ni Kenya Airways (118), Benki ya Standard Chartered (300), Farm Karuturi (2,600), Benki ya Family (100), Telkom (500), Benki ya First Community (100), Benki ya Equity (400), Samir Africa (600), Portland Cement (1,000), Kenya Fluorspar (700), Uchumi (253), Airtel Kenya (80), Kenya Meat Commission (118) na nyengine zinatarajiwa kufuata.

Thamani ya shilingi imeanguka kiasi ikilinganishwa na dollar, hali hii imewepelekea wamililiki wa mitambo ya kusaga kutoa ilani ya kupungua kwa nafaka kutalazimisha kuongezeka kwa bei ambayo itawasukumia wananunuzi madukani kwani bei hiyo itapanda kwa muda mrefu. Licha ya haya yote, Mapato ya Taifa (GDP) la Kenya yalikuwa kwa asilimia 6.2 mwanzoni mwa robo ya pili ya mwaka 2016 na kuongezeka zaidi jambo linaloashiria hali nzuri ya kiuchumi kiasi cha Benki kuu ya dunia ikaiorodhesha Kenya kuwa nchi ya 3 katika nchi zilizoboresha hali ya kufanya biashara nchini mwake na kuongezeka kutoka 21 katika ya nchi 100 zilizonamazingira bora yakufanya biashara. Hii inaonyesha wazi tofauti kati ya nadharia za kiuchumi na uhalisia wa maisha magumu ya mwananchi wa kawaida.

Matajiri wachache wamefaulu kujilimbikizia idadi kubwa ya utajri na kuwafanya wananchi wa kawaida ni wanunuzi tu. Wanawakopesha ili waweze kununua bidhaa msingi ambazo wameziunda kisha kuwafanyisha kazi ili walipe mikopo waliyowakopesha. Njia ya kujinasua na hali hii ni kurudi katika kutumia dhahabu ili kuhifadhi thamani ya pesa za makaratasi na kubadilisha mfumo wa Urasilimali ambao ndio chanzo cha sera msingi za uchumi usiongiliana kiakili na nadharia zilizobuniwa ili kutoa nafasi kwa pengo kati ya masikini na matajiri kuzidi.

**Bakari Mohamed Dziphengo**

**Mwanachama Katika Ofisi ya Habari Hizb ut-Tahrir Kenya**

# Chaguzi za Kidemokrasia Hudunisha Hadhi ya Wanawake




**M**waka wa 2017, ni mwaka wa uchaguzi mkuu nchini Kenya ambapo viongozi wa kisiasa wanashughulika na kuwashughulisha wananchi vikali na matayarisho ya uchaguzi kama huu.Sekta zote za maisha zimechovywa siasa ndani yake.Wananchi na viongozi wote wanaimba wimbo mmoja; ‘Siasa’ ilimradi kila mtu ameshughulishwa kwa njia moja au nyengine na joto la uchaguzi mkuu. Siasa zimepamba moto kila mahali; ni siasa…siasa… kila mmoja apenda kuizungumzia kama isemwavyo na wenyewe ‘asie na mwana aeleke jiwe’.
Viongozi wa vyama tofauti tofauti na wapambe wao wanashughulika sana katika kuzitafuta kura za uchaguzi huu mkuu.Wanafanya kila juhudi ili mambo yawanyookee.Kila watakaloona bora kufanya na la kuendeleza mbele kampeni basi wanaropokwa na kufanya lolote bila kujali chochote. Wamebadilisha sherehe na hafla mbalimbali kama vile matanga, harusi na mazishi kuwa majukwaa ya kisiasa. Wao na wapambe wao wakijaribu kuuza sera zao potofu za kidemokrasia katika majukwaa haya.
Raia na viongozi watarajiwa hawakubakisha lolote ila wamehakikisha kufanya lolote lile ili kufanikisha malengo yao.Wanawake nao pia wametumiwa katika ufanikishaji huo wa malengo yao. Wameingizwa katika ulingo wa siasa na kutumiwa bila wao kujua kama wanatumiwa.Maskini! wanaona ni raha kwani hupewa vijipesa ndani yake, basi hawafikirii athari ya yale wanayoyafanya kwa jina la kupigia debe viongozi wao.

*endelea ukurasa 7*

kutoka ukurasa 6



Mabanati wamebandikwa majina "Warembo na Uhuru" na "Warembo na Joho" wakijinasibisha na viongozi wanaowapigia debe. 'Warembo' hawa kama walivyoitwa hujirembesha na kuzunguka barabarani wakiimba na kucheza ngoma wakiwa nusu uchi hadharani waonekane na kusikika wakiwafanyia kampeni viongozi waliowachagua. Mama zetu na dada zetu wanajidhalilisha barabarani. Wakaivua stara ya Allah (swt) kwa ajili ya kampeni za siasa potofu ya Kidemokrasia.

Demokrasia pamoja na njia zake za kufikia kwenye uongozi ni upotofu mtupu. Imemdunisha mwanamke thamani yake na inazidi kumfedhehesha na tawala za kidemokrasia za kitwaghut. Heshima aliyoekewa mwanamke na Uislamu leo haipo tena, imewavuka wanawake kama nguo inavyovuliwa mwilini. Wanawake wamefanywa leo kama chombo cha sanaa na biashara kuendeleza uchumi wa taifa. Picha za wanawake wakiwa uchi zimesheheni leo kwenye mabango ya biashara. Na sasa wameingizwa uwanjani bila ya mazoezi, wacheze watakavyocheza, iwe ni rafu au vipi bora wafunge mabao. Hivyo basi mwanamke amejisahau, baada ya kujitosa uwanjani, amesahau kama kuna sheria za uchezaji na anacheza atakavyo.


Hilo la kuzungushwa na ngoma na nyimbo haitoshi, wanawake wameshauriwa kuwanyima waume zao haki zao za ndoa mpaka wawaonyeshe kadi zao za kura. Hii harakati ya kutafuta kura imewatia watu wazimu haswa viongozi wanaotaka kuchaguliwa, wanaamua na kufanya chochote kinachowajia akilini bila kujua athari yake ni nini katika jamii. Wanawake nao wamekuwa kama bendera ambayo hufuata upepo.

Haya ni yakutarajiwa kutokamana na nidhamu hii ya Kidemokrasia ambayo imemgeuza mwanamke kama chombo cha matangazo ya biashara. Matangazo yakiwa na wanawake nusu uchi yametapakaa kila mahali. Kweli kabisa mfumo fisadi wa kirasilimali umemdunisha mwanamke. Kila kitu lazima kiwe na ufisadi. Ni wakati sasa sisi Waislamu tusitishe kuunga mkono upuzi huu na kujikita katika majukumu yetu kama Waislamu; maanake tuna mengi ya kujibu kuhusu yanayotokea kwa familia zetu, mama zetu na dada zetu.

Ama tumejitia upofu au uziwi kuhusu mambo haya? Je hatuwaoni kina mama zetu na dada zetu wakijidhilalisha mabarabarani? Tutaulizwa kuhusu haya; tujiandae kutuoa majibu sahihi kwa Allah (swt)) Ni Khilafah kwa Njia ya Utume pekee inayoweza kuwapa hadhi na heshima wanawake wa Ummah huu bora uliotiwa korokoroni na mfumo batili wa Urasilimali ambao umewatoa wanawake katika jukumu lao msingi la kuwa mama na mke; na kuwafanya kuwa vyombo vya kampeni na kutafuta usemi wa kisiasa.

**Mgeni J Salim**

# Siku ya Ukoma duniani: Hadaa nyengine ya Kibepari




Tarehe 30 Januari dunia iliadhimisha siku ya maradhi ya Ukoma duniani. Asili siku hii iliteuliwa kama makumbusho ya kifo cha aliekuwa kiongozi wa India Mahatma Gandhi anayedaiwa kuwa ndiye aliyefahamu vyema umuhimu wa kushughulikia maradhi haya. Wamagharibi wanadai kuwa siku hii ilioanzishwa mwaka wa 1954 ni kuwatambulisha wagonjwa hao waweze kufahamika na kujulikana kama binadamu wanaostahili heshima na kuwapa fursa ya kuchangia jamii kwa vipaji vyao.

Ukoma umeathiri binadamu tangu miaka elfu nyingi zilizopita. Maradhi hayo yamepata jina lake ku-
toka neno la Kilatini lepra, maana yake ni mwenye gamba kwenye ngozi. Pia hujulikana kwa jina la "maradhi ya Hansen" linalotokana na jina la daktari. Ugonjwa huu husababishwa na bakteria vinavyojulikana kitaalamu kama Mycobacterium leprae na M. lepromatosis.

Baada ya ambukizo kuna kipindi ambapo mgonjwa hana dalili za ukoma. Kipindi hicho bila dalili kinaweza kuendelea hadi miaka 5 au zaidi. Dalili zinazoonekana ni kwa mfano vidonge vya chembe vya neva, vya mfumo wa upumuaji, vya ngozi na vya macho. Wakati dalili zinapoanza kuonekana mgonjwa hasikii
tena baridi, joto wala maumivu. Kwa hiyo hatambui kirahisi kama amepata jeraha. Vidonda vinavyotokea havimi na uchafu pamoja na bakteria hatari

endelea ukurasa 8

zinaingia mwilini. Hivyo vidonda vinaweza kuwa vikubwa zaidi kwa sababu havitibiwi au vinachelewa kutibiwa. Ndiyo sababu pengine wakoma wanapoteza viungo vya mwili kama vidole na hata mguu au mkono kutokana na majeruhi yanayorudiarudia.

Dr Erwin Cooremen mkuu wa jumuia ya Global Leprosy Programme alisema kwenye kongamano la Ukoma lilioandaliwa Uchina mwezi Septemba mwaka jana (2016) "Leprosy is not declining at the pace we would like to see," ( Ukoma haupungui kwa kasi tunayopenda kuiona) Akaendelea kusema: "Our new strategy involves leadership and coordination, and focuses not only on medical or public health interventions but also on personal and social aspects – factors that are important for a disease that is still so stigmatized." (Mkakati wetu unahusisha uongozi na ushirikiano na si tu kuangalia madawa ama kushughulikia afya ya umma bali pia kuangalia hali za kibinafsi na jamii- sababu ambazo ni muhimu kwa ugonjwa huu ambao hadi sasa unafanyiwa unyanyapaa).

Kwa haya inadhihirisha wazi kwamba ubepari kimakusudi haujatabani/kuchukua kidhati suala la maradhi haya. Ndio hadi wa leo maradhi haya yanaendelea kuwa sugu huku India pekee ikiwa na asilimia 60 ya wanaougua maradhi haya kote duniani.

Hadaa za mabepari katika kushughulikia maradhi: Kuwekwa siku kama hizi na mfano wake ni kujaribu tu kuhadaa watu waamini kuwa Urasilimali kweli unajali umma. Warasilimali licha ya kupiga hatua katika utengezaji wa madawa nalo ni jambo zuri linalohimizwa na Uislamu, lakini wao huangalia suala la afya kwa hesabu za manufaa ambayo ndiyo kipimo chao cha kusukuma harakati na mienendo ya wanadamu. Hawaangalii afya kwa msingi kuwa ni hitajio muhimu la kibinadamu bali huliangalia kwa msingi wa tija ya kiuchumi yaani; Je watu ambao afya zao zikiangaliwa zitaleta faida ya kiuchumi. Hivyo watu ambao kwa warasilimali hawajakuwa na umuhimu wa kiuchumi kwao afya zao hudunishwa kwa kunyimwa matibabu na madawa. Ndio maana kauli mbiu ya shirika la Afya duniani imekuwa; 'Afya na Maendeleo'. Aidha, warasilimali na serikali zao huchukua huduma ya afya kama fadhila kwa raia wake wala sio kama jukumu lao kwa umma.

Ufahamu sahihi kuhusu uzima na maradhi: Katika Uislamu afya huangaliwa kama neema kubwa kwa mwanadamu anayofaa kwayo kumshukuru Allah SWT. Ndio katika mafundisho ya Uislamu tukashajiishwa kutafuta dawa kama ilivyopokelewa kutoka SAAW… akisema:

**فعن أسامة بن شريك عن النبي صلى الله عليه وسلم أنه قال:**

**((تداووا يا عباد الله فإن الله لم يضع داء إلا وضع له شفاء إلا داء واحدا الهرم))**

**"Tafuteni dawa enyi waja wa MwenyeziMungu kwani MwenyeziMungu hakuweka maradhi ila iko dawa yake ispokuwa Uzee hauna dawa."**

Isitoshe Uislamu ukajaalia kuwa matibabu ni mmoja wapo ya mahitaji msingi ya jamii/umma na ni jukumu la serikali kuhakikishia rai wake haki hii. Moja katika fahamu za Kiislamu kuhusu matendo ya mwanadamu ni kuwa yapo matendo ambayo hutukia kwa mwanadamu pasina na khiyari yake yaani hutukia pasina matakwa yake haya huitwa Qadhaa yaani MwenyeziMungu pekee ndie aliyeamua kutukia kwake mfano ni Maradhi. Mwislamu hivyo hutakikana kila anapougua maradhi basi atafute dawa lakini wakati huo huo awe na subra kwa kuelewa kua hiyo ni kadhaa ya Allah lau ataisubiria atapata ujira mkubwa.

**عَنْ أَبِي سَعِيدٍ الْخُدْرِيِّ وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ (رضي الله عنهما) عَنْ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: ((مَا يُصِيبُ الْمُسْلِمَ مِنْ نَصَبٍ وَلاَ وَصَبٍ وَلاَ هَمٍّ وَلاَ حُزْنٍ وَلاَ أَذًى وى غَمٍّ حَتَّى الشَّوْكَةِ يُشَاكُهَا إِلاَّ كَفَّرَ اللَّهُ بِهَا مِنْ خَطَايَاهُ))**

Kutoka kwa Abu Sa'iyd Al-Khudriyy na Abu Hurayrah (رضي الله عنهما) kwamba Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) amesema:

**"Muislamu hatopatwa na tabu, wala maradhi, wala hamu wala huzuni wala udhia wala ghamu [sononeko] hata mwiba unaodunga isipokuwa Allaah Humfutia madhambi yake kwa sababu ya hayo"**

Al-Bukhaariy na Muslim

Muhimu pia kufahamu kuwa kukithiri ufisadi na maasia kwa ujumla hupelekea watu kupata magonjwa. Leo twaishi chini ya mfumo fisidifu wa kirasilimali unaofungua mlango wa kumkufuru na kumuasi MwenyeziMungu tusitarajie kuwa salama. Isitoshe mfumo wa kibepari umezalisha matatizo ya kiuchumi, kisiasa na kijamii kiasi cha jamii kuzongwa na mawazo yanayosababisha maradhi ambayo hayakuweko katika zama za Uislamu ulipokuwa ukiendesha dunia kupita Khilafah yake. Kwa mfano shirika la Afya duniani limekiri kuwa msongo wa mawazo leo umesababisha maradhi ya vidonda vya tumbo na pressure. Imepokewa kuwa Mtume SAAW amesema

**((من كثُرَ همُّهُ سقمَ بدنُه))**

**"Mwenye kuwa na shida/hamu? nyingi basi mwili wake huugua"**

Maradhi kama mtihani kwetu: Familia nyingi leo hufeli kuelewa kuwa maradhi pia ni sehemu ya Mitihani kwetu kutoka kwa Mola wetu. Imani hii ni muhimu sana kwani ikikosekana watu huingia katika kufuru na ushirikina kwa sababu ya maradhi. Kiislamu tumehimizwa mno kuwa na subra. Hapa ndio huja suala la unyanyapaa yaani kutengwa kwa mwenye maradhi kama vile ukoma, ukimwi na mengineyo. Na hili limekuwa tatizo la wazi katika mfumo wa kibepari kama inavyodhihirika kutengwa kwa wagonjwa katika makambi ya wa ukoma. Katika nchi kama India makambi hayo yapata zaidi ya elfu. Pia China na Afrika makambi haya yanapatikana kwa mia kadha. Katika historia ya Ukoma utakuta kuwa umesababisha wagonjwa wake kubaguliwa kwa miaka mingi. Ubaguzi huo bado ndio huhamasisha wagonjwa kujificha na kukosa matibabu mapema. Na hapa napenda ifahamike kuwa maana ya kumbagua mgonjwa wa ukoma ni kule kutomshughulikia kimatibabu na kumdharau. Ama kutahadhari na wenye ugonjwa huu ili kuepuka maambukizi hili haliingii kwenye unyanyapaa bali ni katika mafunzo ya Uislamu pale SAAW aliposema:

**((فر من المجذوم كما تفر من الأسد))**

**"Kumkimbia mwenye ukoma ni kama kumkimbia samba"**

Kwa haya twasema umma utaendelea kupuuzwa kila unapo kumbwa na maradhi kwa kuhadaiwa na 'mashirika' ya kirasilimali ambayo yenyewe hutaka watu waugue bali husaidia kusambaza maradhi kwa watu wa kawaida ili wapate kuuza madawa ambayo kiasili si yenye kutibu kikweli ila kuleta afueni tu ya muda. Kusimamishwa Uislamu kupitia serikali yake halisi ya Khilafah ndio pekee kutashughulikia umma matatizo yake kikweli.

**Shabani Mwalimu**
**Mwakilishi kwa Vyombo vya Habari**
**Hizb ut-Tahrir Kenya**